* HABARI LEO UK 5.

# Sekta binafsi kichochezi kupungua gharama vyakula vya mifugo

Na Mwandishi Wetu

UWEKEZAJI, Teknolojia, Ubunifu na Ushirikishwaji kikamilifu wa sekta binafsi utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ongezeko la gharama ya bei ya vyakula vya mifugo na kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchini.

Imeelezwa kwamba gharama za uzalishaji wa vyakula vya mifugo ndio kichocheo cha kupanda kwa bei ya mifugo hiyo sokoni kama vile samaki, ng'ombe, kuku na aina nyingine za mifugo kulinganisha na nchini jirani.

Akizungumza katika kongamano la siku moja la umuhimu wa kuongeza ushindani katika sekta ya vyakula vya mifugo vyenye protini, iliyoandaliwa na ubalozi wa Uholanzi hapa nchini kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kusini Mwa Tanzania (SAGCOT) mwishoni mwa wiki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema kwamba ni muhimu kwa kuvutia uwekezaji kwenye sekta hiyo ili kuleta mabadiliko.

"Pamoja na mambo mengine ni muhimu kwa taasisi za fedha hasa benki hapa nchini kuanza kutoa mikopo kwa wazalishaji wa vyakula vya mifugo ili kuvutia wadau wengine kuingia kwenye sekta hii," alisema.

Aliongeza kwamba ni muhimu kuwe na malisho bora yenye viwango vya ajili ya mifugo ili kuweza kuifanya sekta iwe shindani ndani ya soko la Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla na kuendelea kuvutia uwekezaji zaidi kutoka nje.

"Nachukua nafasi hii kuwaelekeza Wakala wa Maabara ya Veterinari (TVLA) kuanza utaratibu wa kuwafuata wazalishaji wa vyakula vya mifugo ambao wana viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo na kuwakagua na kujiridhisha kwamba wanauza vyakula vyenye ubora unaotakiwa," aliongeza.

Alisisitiza ni muhimu kwa wakala huyo wa serikali kuanza programu hiyo ya kuwatembelea wazalishaji wa vyakula vya mifugo ili kuwatambua wote ambao wamesajiliwa na kampuni yao kama wazalishaji wa vyakula vya mifugo hapa nchini na kuwapa mwongozo pamoja na kuwasaidia kuweza kufikia viwango vya kimataifa vya ubora.

"Unajua gharama za vyakula vya mifugo hapa nchini zipo juu kwa mfano bei ya sato ni mara mbili na jirani zetu Kenya na hii inatokana na vyakula vya mifugo bei yake kuwa juu," alifafanua.

Alisema kwa sasa kwa takwimu zilizopo kuna kampuni 223 yaliyosajiliwa yanayotengeneza vyakula vya mifugo hapa nchini kwa njia ya kitaalamu lakini kuna wengi bado wapo kila kona na ni jukumu la Wakala wa Maabara ya Veterinari kuweza kuwatambua na kuwapa mwongozo pamoja na mambo mengine kuchukua hatua za kisheria inapobidi.

Kwa upande wake, Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer alisema: "Kongamano hili ni muhimu kwa wadau wote katika sekta hii muhimu la vyakula vya mifugo kwa sababu gharama zinapanda siku hadi siku na ni muhimu kwa watafiti na wadau wengine kuja na njia mbadala wa kupunguza gharama hizo".

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu SAGCOT, Geoffrey Kirenga alisema kwamba sekta ya vyakula vya mifugo hapa nchini ni muhimu kwa kilimo na uchumi wa nchini kwa ujumla.

"Utajiri wa rasilimaliwa mifugo kama vile ufugaji wa kuku wa biashara hapa nchini inakadiriwa kufikia 72 milioni, huku milioni 28.9 ng'ombe, milioni 16.7 mbuzi na million 5.0 kondoo," alisema.

Akiwasilisha mada ya chakula mbadala cha mifugo chenye protini, Profesa Faustine Lekule alisema kwamba moja ya protini mbadala ni kuhamasisha wakulima kulima soya maana ina manufaa kwa chakula cha mifugo na binadamu hapa nchini.

CamScanner



Mkazi wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma akiwa na mbwa wake wakati wa maadhimisho ya siku ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

HABARI LEO UK 13.

# 'Serikali imekaa 'siti ya mbele' kumaliza kichaa cha mbwa nchini

Inatoka 9

kwa dakika au zaidi kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni na kidonda kisifungwe kisha apelekwe haraka kituo cha kutolea huduma za afya ili kupata chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa," anasema Warioba.

Pia ni muhimu aliyeng'atwa na mbwa afanyiwe tathmini ya kina katika kituo cha kutolea huduma ili aweze kupatiwa chanjo kamili na iwapo chanjo itatolewa mtu hana budi kumaliza dozi zote za chanjo zinazotakiwa.

"Wanyama jamii ya paka wasiruhusiwe kulamba vidonda kwani mate yao huleta maambukizi endapo wameathirika."

Anashauri wamiliki wa mbwa wahakikishe wanachanja mbwa wao dhidi ya ugonjwa huo mara moja kila mwaka ili wasipate maambukizi.

"Mbwa wafungiwe ndani wakati wa mchana na wasizurure hovyo kwani wanaweza kupata maambukizi endapo watakutana na mnyama aliyeambukizwa," anasema.

Pia anataka watoto wapewe elimu na wakatazwe kuchokoza mbwa wanaozurura mfano kuvuta mkia, masikio na hata kupanda mgongoni.

Mkurugenzi Msaidizi wa Afya ya Mifugo Ngazi ya Jamii, Stanford Ntabalema anasema ugonjwa huo huishi kwa baadhi ya wanyama wa porini ikiwemo popo ambapo husambaa kupitia wanyama wa nyumbani kwa kuambukizwa.

"Mbwa na wanyama wengine wenye virusi vinavyosababisha kichaa cha mbwa huambukizwa bila kuonesha dalili zozote, hivyo ni muhimu mtu yeyote aking'atwa na mbwa au mnyama mwingine atoe taarifa kwa mtaalamu wa mifugo ili hatua husika zichukuliwe," anasema Ntabalema.

Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dk Robert Kishimba anasema mbali na juhudi za kuutokomeza ugonjwa huo bado ni janga na hivyo ni lazima kuuepuka.

Mtaalamu wa magonjwa ya mbwa ambaye pia ni Ofisa Mifugo Wilaya ya Kongwa, Dk Kisimba Benjamin anasema ugonjwa wa kichaa cha mbwa huanza kipindi cha baridi.

Anataja dalili zake kwa binadamu ni pamoja na homa, kuumwa kichwa, kuwashwa sehemu ya jeraha, maumivu ya mwili, kuchanganyikiwa na kuvunja, kupiga vitu na kuogopa mwanga.

Pia kubweka kama mbwa, kuogopa maji, ikiwemo maji ya kunywa, kutokwa na mate mengi mfululizo, kuweweseka na kushtuka mara kwa mara, kupooza, kudhoofu na hata kupoteza maisha.

Tanzania inakadiriwa kuwa na mbwa takribani milioni 4.5 na paka milioni mbili wanaofugwa kwa malengo mbalimbali na kwa mwaka kuna wastani wa matukio 2,030 ya mbwa wanaodhaniwa kuwa na kichaa.

Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya za Wanyama duniani (WOAH) na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) kwa pamoja wamekubaliana kutokomeza ugonjwa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule anasema: "Kila mtu ambaye anafuga mbwa lazima afuate sheria na taratibu zake, naagiza wataalamu wa mifugo wa wizara na sekretarieti kutafuta suluhu ya mbwa wote wanaozurura mitaani. Mtu kama hawezi kufuata sheria, aache kufuga wanyama hao."

Anasema ugonjwa wa kichaa cha mbwa husababisha vifo 1,500 kila mwaka nchini na watoto chini ya miaka mitano ndio wamekuwa waathirika wakubwa.

Senyamule ametaja lengo la dunia ni kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa ifikapo 2030 kwa kuhakikisha kila mbwa anapatiwa chanjo kila mwaka.

"Naomba utaratibu huu uwe endelevu mpaka ugonjwa huu uwe historia kwani Tanzania bila kichaa cha mbwa inawezekana. Tunatakiwa kuzingatia chanjo na kupunguza idadi ya mbwa tunaofuga," anasema Senyamule.

Maadhimisho ya utoaji chanjo kwa mbwa na paka hufanyika kila mwaka duniani ikiwa ni kumuenzi muasisi wake Dk Luis Paster ambaye ndiye aligundua chanjo hii kwa wanadamu na mbwa kwa mara ya kwanza mwaka 1885.



Mbwa akipewa chanjo kuzuia kichaa cha mbwa na magonjwa mengine

GHARAMA

MWANANCHI UK 22.

# Mwarobaini bei za vyakula vya mifugo

Sute Kamwelwe, Mwananchi
skamwelwe@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Uwekezaji, teknolojia na ushirikishwaji kikamilifu wa sekta binafsi vimetajwa kuwa mwarobaini wa kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ongezeko la gharama ya bei ya vyakula vya mifugo na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchini.

Imeelezwa gharama za uzalishaji wa vyakula vya mifugo ndio kichocheo cha kupanda kwa bei ya mifugo hiyo sokoni kama vile samaki, ng'ombe, kuku na aina nyingine za mifugo kulinganisha na nchini jirani.

Akizungumza na washiriki wa kongamano la siku moja la umuhimu wa kuongeza ushindani katika sekta ya vyakula vya mifugo vyenye protini, iliyoandaliwa na Ubalozi wa Uholanzi hapa nchini kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kusini Mwa Tanzania (SAGCOT) mwishoni mwa wiki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema ni muhimu kuvutia uwekezaji kwenye sekta hiyo ili kuleta mabadiliko.

"Wadau wote wanakutana kujadiliana na kuja na mapendekezo namna bora ya kupunguza gharama ya bei ya vyakula vya mifugo kwa kuongeza ubunifu, uwekezaji na teknolojia ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi, ukame, mitaji na changamoto nyingine za kibinadamu," alisema.

Ulega pia alisema Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikuja na sheria ya malisho na rasilimali ya vyakula vya mifugo ili kusimamia kikamilifu sekta hiyo.

"Nachukua nafasi kuwaelekeza Wakala wa Maabara ya Veterinari (TVLA) kuanza utaratibu wa kuwafuata wazalishaji wa vyakula vya mifugo ambao wana viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo na kuwakagua na kujiridhisha wanauza vyakula vyenye ubora unaotakiwa," aliongeza Waziri Ulega.


Kwa upande wake, Balozi wa Uholanzi hapa nchini, Wiebe de Boer alisema kongamano hilo liliwaleta pamoja watunga sera, watafiti, Serikali, wadau wa sekta husika na wazalishaji wa vyakula vya mifugo kukaa pamoja na kujadiliana jinsi ya kuja na suluhisho la kupunguza gharama za vyakula vya mifugo nchini.

"Kwenye sekta hii mazao na ufugaji ambayo kwa jumla yanabeba maisha, kipato na ajira kwa zaidi ya asilimia 80 ya idadi ya watu nchini ni muhimu kuangaliwa kwa jicho la kipekee ili kutoa matokeo chanya na hizi gharama zinazopaaa kila siku zipatiwe majawabu," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu SAGCOT, Geoffrey Kirenga.

Aliongeza kuwa utajiri wa rasilimali wa mifugo kama vile ufugaji wa kuku wa biashara nchini inakadiriwa kufikia milioni 72, huku ng'ombe million 28.9 , mbuzi million 16.7 na kondoo milioni 5.

**NUKUU**

"Kwenye sekta hii mazao na ufugaji ambayo kwa jumla yanabeba maisha, kipato na ajira kwa zaidi ya asilimia 80 ya idadi ya watu nchini ni muhimu kuangaliwa kwa jicho la kipekee ili kutoa matokeo chanya na hizi gharama zinazopaaa kila siku zipatiwe majawabu." Geoffrey Kirenga



more re- ing. gender equality and women

THE GUARDIAN Page 4

# ...ncer

...h include
...e.
...invest in
...areness so
...h compre-

...aid the in-
...mmence a
...e following
...itron emis-
...otron (PET/

...s of money
...he service
...e East Afri-

...d it is more
...g tests pro-
...cancers.
...te is imple-
...nd expand

...liamentary
...overnment
...s including

...enses were
...why many
...edical spe-

...to effective
...ices in hos-

...000 deaths
...rs occur in
...ex and age.
...ur in men.




Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega (2nd-R) receives a gift from the Netherlands Ambassador to Tanzania, Wiebe de Boer, at a workshop on fostering competitiveness in Tanzania's feeds sub-sector with a focus on protein ingredients. It was held in Dar es Salaam late last week, jointly organised by the Netherlands Embassy and the Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT). Looking on are SAGCOT chief executive officer Geoffrey Kirenga (L) and Dr Nazaeli Madalla, a director in the Livestock and Fisheries ministry. Photo: Guardian Correspondent

...high in Tanzania, says new report

*Officer, Ruth Zaipuna, Director of Diaspora Affairs at the Ministry of Foreign Affairs and East African Cooperation, Amb James Bwana (right), Chief of Retail Banking, Filbert Mponzi (left) and the Tanzanian Ambassador to the United Kingdom, Mbelwa Kairuki at a ceremony in Dar es Salaam, over the weekend. (Photo by a Correspondent)*

DAILY NEWS, Page 16

# Reduce animal feed prices, Ulega tells producers

**By DAILY NEWS Reporter**

INVESTMENT attraction, adoption of emerging technologies, innovation and participation of the private sector are among the key factors that can reduce the cost of price of animal feeds and foster competitiveness in the country.

Speaking to participants during a one-day workshop organised by the Dutch Embassy in collaboration with Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT) in Dar es Salaam over the weekend, Minister for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega said it was important to attract investments in the production of animal feeds and encourage competition.

He explained that the cost of production of animal feeds was hiking the price of fish, chickens and other types of livestock compared to neighbouring countries such as Kenya.

"All stakeholders are meeting here today to discuss and come up with suggestions on the best way to reduce the cost of price of animal feeds by increasing creativity, investments and adopting emerging technologies so that we can address climate change, prolonged droughts and finances and other challenges," he said.

He called on financial institutions, especially banks in the country, to start issuing loans to producers of animal feeds and make their business sustainable.

"Let me take this occasion to direct the Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA) to start making follow-ups to producers of animal feeds who have factories and inspect them if they sell high quality animal feeds," said Minister Ulega.

He emphasised that it was important for the TVLA to start a programme of visiting producers of animal feeds to identify those who were registered with their companies as producers of animal feeds in the country, guide and help them produce feeds that met international standards.

"You are all aware that the cost of production of animal feeds in this country is high. For instance, the price of tilapia has doubled compared to neighbouring Kenya and this is due to the cost of price of animal feeds," he said after opening the workshop and answering to journalists' questions.

He said currently Tanzania had at least 223 registered feed mills, with only 15-20 of them operating at professional and commercial levels.

For his part, Netherlands Ambassador to Tanzania Wiebe de Boer said the one-day workshop brought together policy-makers, researchers, the government, livestock and fisheries stakeholders and the producers of animal feeds to sit together and develop a road map on achieving competitiveness in the production of animal feeds.

"This workshop has come at the right time when the cost of production of animal feeds is increasing day by day, which poses a threat to all actors.

It is high time all stakeholders came up with alternative sources of protein to reduce the cost of production of animal feeds," said Ambassador de Boer.

"Apart from reflecting this workshop will pave the way for all actors to stimulate resilience for the feed sector in the near future that will create immense opportunity," he added.

Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT) Chief Executive Officer Geoffrey Kirenga said the animal feed industry in the country held a central position in agriculture and in the economy of the country.

"It is the intersection of both crop production and livestock rearing systems, which collectively provide livelihoods, income and employment for over 80 per cent of the population," he said.

Presenting a paper on the findings and recommendations of a study on alternative sources of proteins, Prof Faustine Lekule said one of the alternative sources of proteins was to encourage farmers to grow soybean because it was beneficial for animal and human consumption in this country.

CamScanner

NIPASHE UK5

# Mpango mpya wa lishe bora kutoka Yara Tanzania kukuza tija sekta ya mifugo, uvuvi



Mkuu wa Mkoa wa Iringa Halima Dendego na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya Yara Winstone Odhiambo wakizindua rasmi bidhaa za lishe ya mifugo iliyo tambulishwa na kampuni hiyo katika hafla iliyofanyika mjini Iringa juma lililopita



## Bidhaa mpya za lishe ya mifugo kutoka Yara Tanzania

1. **Kynofos 21** Ni bora kwa broilers na kuku wa mayai, samaki, nguruwe na wanyama kama paka;

Faida
- Inaongeza kiwango cha ukuaji kwa wanyama.
- Inaongeza uzalishaji na mayai.
- Inaimarisha ubora wa ganda la yai.
- Inaboresha ututoleshaji wa vifaranga.

2. **Maziwa Pro** ni mahususi kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa. Ina Kiwango kikubwa cha chembechembe za madini ya Phosphorus. Pia imerutubishwa na sukariguru na asilimia 15 ya protini.

**Faida**
- Inaongeza uzalishaji na ubora wa maziwa.
- Inachochea joto la kupandwa na kushika mimba.
- Kuzuia ulaji ovyo wa mifuko ya plastiki na vitu vya jamii ya miti/mbao.
- Inaongeza kinga ya mwili na kupunguza changamoto za magonjwa.

3. **Kalori 3000** ni bidhaa ya unga mkavu wa kunyunyiziwa sukariguru (Molasses)

**Faida**
- Kuongeza ladha na ulaji wa chakula.
- Kuboresha umeng'enywaji wa chakula kwa wanyama wanaocheua.
- Inaimarisha kuchachushwa kwa majani yaliyovundikwa [Silages]
- Inahakikisha usahihi wa ubora wa madini kwenye jiwe la kulamba.
- Huongeza uzalishaji kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inachochea unenepaji wa haraka kwa mifugo wa nyama.

4. **Feed Grade Urea** ni chakula ambacho ni chanzo rahisi cha protini kwa ajili ya wanyama wanaocheua

**Faida**
- Huboresha ukuaji wa Wanyama.
- Huboresha umeng'enywaji wa chakula, nyasi kavu.
- Huongeza uzalishaji wa maziwa.
- Inachochea unenepaji wa haraka kwa mifugo wa nyama.

5. **Kimtrafos 12 Grande** ni chakula cha Phosphate yenye wingi wa madini madogomadogo mahususi kulisha ng'ombe (wa nyama na maziwa), kondoo na mbuzi.

**Faida**
- Ina madini yote madogomadogo katika uwiano ulio sahihi kwa phosphorus.
- Haina vumbi ili kurahisiha maandalizi na uchanganyaji
- Ina sukariguru (molasses) ya unga ili kuongeza ladha na ulaji wa phosphorus.
- Inaongeza kiwango cha uzalishaji maziwa.

6. **Phospro 17** Ni Phosphate ya chumvi na protini kwa ajili ya chakula cha mifugo. Nzuri kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama pori wanaofugwa wakati wa kiangazi au wanaolishwa majani makavu.

**Faida:**
- Ina zaidi ya madini 8 na kuboreshwa na sukariguru ya unga yenye 17% protini.
- Inaboresha umeng'enywaji chakula na hamu ya kula wakati wa kiangazi.
- Inaimarisha ukuaji na uzazi wa mifugo.
- Stahimilivu kwa hali ya hewa na inaweza kuwekwa nje kwenye mvua.

7. **Feed Grade Sulphur** ni chakula cha mifugo ambacho kina Sulphur inayosaidia wanyama wanaocheua kuchakata amino asidi, methionine na lysine.

**Faida**
- Huongeza uzalishaji maziwa kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inaongeza kiwango cha uzazi na ndama wenye afya
- Inaboresha ngozi na mwonekano angavu wa mnyama.
- Kupunguza hatari ya magonjwa.
- Huongeza ufanisi wa matumizi ya urea ya chakula cha mifugo.

Na mwandishi wetu

Kutambulishwa katika soko la Tanzania kwa aina mpya ya bidhaa bora za lishe ya mifugo kutoka Yara bila shaka kutakuwa ni hatua muhimu katika maendeleo ya sekta ya mifugo na uvuvi nchini. Uzinduzi wa bidhaa saba za kiwango cha juu na himilivu katika mazingira kwa mifugo, kuku na ufugaji wa samaki uliofanywa na Yara Tanzania Septemba 19, 2023, umeonyesha kwa vitendo dhamira ya kampuni hiyo katika kuchangia usalama wa chakula nchini, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kanuni bora za kilimo zenyetija.

Ujio huo wa aina mbalimbali za vyakula vya mifugo kutoka Yara utaleta maendeleo chanya kwa Tanzania, na imekuja mara baada ya Tanzania kuandaa Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) lililofanyika mapema mwezi Septemba kwa mafanikio makubwa.

AGRF pia ni jukwaa kuu la dunia la kilimo na mifumo ya chakula barani Afrika.

Mkutano huo uliwaleta pamoja zaidi ya wadau 5000 kuchukua hatua za kiutendaji na kuchochea mawazo yanayolenga kuendeleza mifumo ya chakula Afrika.

Yara International ni mshirika mkuu wa AGRF na inafanya kazi katika nchi zaidi ya 160, ikiwa ni pamoja na Afrika, ikifanya kazi na mamilioni ya wakulima kushughulikia changamoto za uzalishaji na ustawi wao.

"Kwa kuingia katika soko la lishe ya mifugo, Yara Tanzania inaiishi dhamira ya AGRF na pia kuendele- za azma yake kimataifa ya "Kukuza kilimo endelevu, ustawi shirikishi na kuhimili mabadiliko ya tabianchi," anasema Winstone Odhiambo, Mkurugenzi Mkuu wa Yara Tanzania na Rwanda.

Mpango wa Yara ni kuwawezesha zaidi ya wakulima milioni 50 ifikapo 2030 duniani kote. Tanzania na Rwanda ni nchi za tatu na nne barani Afrika mtawalia kuanzisha suluhisho ya lishe ya mifugo baada ya Afrika Kusini na Kenya.

Yara ni watengenezaji wa kimataifa wa vyakula bora vya mifugo kwa kiwango cha ubora wa kimataifa katika viwanda vyake vya uzalishaji vilivyopo Kokkola (Finland) na Durban (Afrika Kusini) ambavyo husambazwa katika nchi 70 duniani.

"Bidhaa zetu mpya za lishe ya mifugo zitaleta athari chanya katika ufugaji kwa kuboresha afya ya mifugo, kuongeza uzalishaji wa nyama, maziwa, mayai na samaki, na pia kupunguza athari za mazingira zinazotokana na ufugaji.

"Dhamira yetu ni kuwawezesha wakulima kustawi huku tukichangia maendeleo endelevu," anasema bwana Odhiambo, na kuongeza kuwa wasindikaji wa vyakula vya mifugo pia watafaidika na mchanganyiko wa lishe ya mifugo ya Yara ili kuboresha ubora wa bidhaa zao.

"Hii kwetu sio ajenda ya ushindani ila tunatoa fursa ya kushirikiana kuleta mageuzi makubwa katika soko la chakula cha mifugo kwa faida ya wakulima, wauza bidhaa na uchumi kwa ujumla." Wafugaji na wazalishaji wa vyakula vya mifugo wamekaribisha Yara katika soko la chakula cha mifugo ili kukabiliana na uhaba na ubora duni wa bidhaa hizo ambao umekuwa changamoto kubwa.

Bidhaa chache na duni za lishe za mifugo zimerudisha nyuma tija na kuvuruga mnyororo mzima wa thamani.

> "Tunafuraha kuwa Yara Tanzania inaleta bidhaa za vyakula vya mifugo vyenye virutubisho vingi. Tuko tayari kutoa maarifa ya bidhaa hizi ili kuwasaidia wafugaji wadogo kuongeza tija."
>
> **FAUD ABRI** | Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ASAS Dairies ya Iringa.



Changamoto zinazozidi kuongezeka za janga la Uviko-19 na kupanda kwa bei ya nafaka wakati wa vita nchini Urusi na Ukraine kulizidisha hali hiyo, huku wakulima walioelemewa na mizigo wakilazimika kuachana na vyakula vinavyozalishwa viwandani na badala yake kuelekeza rasilimali nyingi katika kuzalisha vyakula wenyewe. "Tunafuraha kuwa Yara Tanzania inaleta bidhaa za vyakula vya mifugo vyenye virutubisho vingi.

Tuko tayari kushirikiana na Yara kutoa maarifa ili kuwasaidia wafugaji wadogo kuongeza tija," alisema Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ASAS Dairies ambayo ni wazalishaji na wasindikaji wakubwa wa maziwa nchini, bwana Fuad Abri alipokuwa mwenyeji wa timu ya viongozi wa Yara Tanzania walipotembelea ofisi na mashamba ya kampuni hiyo mkoani Iringa.

Abri alisema ni wakati wa kuunga mkono juhudi kama wafanyabiashara wenye lengo moja la kubadilisha fikra za wakulima ili wafuge kisasa, kwa ubora na uendelevu.

Licha ya kuwa nchi ya tatu barani Afrika kwa idadi kubwa ya mifugo, Tanzania ina upungufu wa uzalishaji wa maziwa lita bilioni 9 kila mwaka, ikitumia zaidi ya Sh 30 bilioni kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ili kufidia pengo hilo.

Wafugaji wadogo mkoani Iringa, Baraka Kibugu, Majoeno Ziangi na Simeon Kikoti walionyesha matumaini kuwa bidhaa hizo mpya za Yara zitaboresha uwekezaji wao.

"Tuna uhakika kwa sababu Yara ina chapa bora za mbolea na imejijengea sifa ya kushirikiana na wakulima na wasambazaji," alibainisha Kikoti.

Kwa upande wake Ziangi alisema; "Kupatikana kwa lishe bora kutabadilisha uwekezaji wangu.

Tunatoa wito kwa Yara kuzingatia vifungatio vidogo vya chakula cha mifugo vya bei nafuu kwa wafugaji wengi wadogo.

Tunafurahi kuwa bidhaa hizo zinakuja na viwango vya ubora vilivyothibitishwa kimataifa." Bwana Odhiambo alisema Yara Tanzania itahakikisha kuwepo kwa vifungashio ambavyo wafugaji wakawaida watavimudu kupitia mawakala wao waliopo maeneo mbalimbali nchini.

CamScanner

TAIFA




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia), akikabidhiwa zawadi na Balozi wa Netherlands hapa nchini, Wiebe de Boer (wa pili kushoto), katika warsha ya siku moja kuhusu umuhimu wa kuongeza ushindani kwenye sekta ya vyakula vya mifugo vyenye protini iliyoandaliwa na ubalozi huo kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Geoffrey Kirenga na Mkurugenzi wa Ufugaji wa Samaki kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazaeli Madalla (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**